

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA

(Mawasiliano yote yafanywe kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)

MKOA: NJOMBE

Simu +255 – 26 2790120
Fax +255 – 26 2790128
Barua pepe : ded@ludewadc.go.tz
Tovuti : www.ludewadc.go.tz
KUMB.NA.LDC/L.10/13 VOL.IV/111



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S.L.P 19,
Ludewa,

25/09/2017

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa anapenda kuwataarifu waombaji wote wa nafasi za kazi ya Mtendaji wa kijiji Daraja III (nafasi 58) na Msaidizi wa hesabu (nafasi 3) kuwa usaili utafanyika tarehe 7 - 9 Oktoba, 2017 katika ukumbi wa shule ya Sekondari Chief Kidulile iliyopo karibu na Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kuanzia saa 1.30 Asubuhi.

Wasailiwa mnapaswa kuzingatia maelezo yafuatayo:-

- I. Kila msailiwa anawajibika kuzingatia muda na kituo cha usaili kama ilivyoainishwa.
- II. Kila msailiwa anapaswa kuwa na kitambulisho kwa ajili ya utambuzi.
- III. Vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na **Kitambulisho cha makazi, kitambulisho cha mpiga kura, kitambulisho cha kazi, kitambulisho cha uraia au hati ya kusafiria.**
- IV. Wasailiwa mnatakiwa kufika na vyeti halisi (**Original**) vya kuzaliwa, Astashahada(Cheti),Cheti cha kidato cha nne na kuendelea kulingana na sifa za mwombaji.
- V. Kila msailiwa atajigharamia kwa chakula, usafiri na malazi.
- VI. Kwa wale waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (**TCU,na NECTA**)kulingana na ngazi ya cheti
- VII. Waombaji kazi ambao majina hayakuonekana katika tangazo hili watambue kuwa hawakukidhi vigezo, hivyo wasisite kuomba tena pindi nafasi za kazi zitakapotangazwa.

Naambatanisha na orodha ya majina ya wasailiwa.


Gilbert Ngailo,

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W),
LUDEWA

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
Ludewa

N.B:Tangazo hili pia linapatikana katika Tovuti ya www.ludewadc.go.tz